JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI

30 JUNI 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI – TAREHE 30 JUNI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya

Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

141. MHESHIMIWA LOLESIA JEREMIAH MASELLE BUKWIMBA (BUSANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Barabara ya Nyakagomba – Katoro kupitia Inyala inayohudumia Kata zilizoko katika

Tarafa ya Butundwe husafirisha mazao na bidhaa za biashara, lakini barabara hiyo haipitiki katika majira yote hivyo kuwafanya wananchi wa maeneo husika kushindwa kufanya shughuli zao za maendeleo, na Halmashauri husika imeshindwa kulitatua tatizo hilo kutokana na bajeti finyu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipandisha hadhi barabara hiyo iwe ya Mkoa ili iweze kuhudumiwa Kimkoa na kumaliza tatizo hilo kabisa.

142. MHESHIMIWA ANIA SAID CHAUREMBO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Halmashauri nyingi nchini zipo katika mchakato wa ujenzi wa Ofisi za Watendaji Kata, na katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna baadhi ya maeneo ya Kata hayana nafasi ya viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo:-

(a) Je, hali ya ujenzi wa Ofisi za Watendaji Kata nchini ukoje;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Halmashauri zenye shida ya kupata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi hizo za Watendaji Kata.

WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:

143. MHESHIMIWA JOHN PAUL LWANJI (MANYONI MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana:- Serikali ya Uganda ilitangaza kuandaa Mkakati wa kupambana na tatizo la ajira kwa wahitimu wote wa Vyuo Vikuu watakaokosa nafasi kwenye Soko la Ajira nchini Uganda na kuwapatia Mikopo ya mitaji ili waanzishe biashara zao, tatizo ambalo pia lipo Tanzania tena kwa kiasi kikubwa:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya kuiga mkakati huo mzuri wa Serikali ya Uganda;

(b) Je, Serikali inaweza kupeleka wataalamu Uganda au nchi nyingine

kujifunza juu ya mkakati huo ili kuondoa tatizo hilo;

(c) Je, Serikali haioni kwamba, kuwaacha wahitimu kujihangaikia ajira wenyewe kunasababisha wakimbilie nchi nyingine (*brain drain*).

144. MHESHIMIWA JAMES PHILIPO MUSALIKA (NYANG'HWALE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana:- Kwa kipindi cha miaka minne sasa Serikali imekuwa ikiahidi kuwakopesha kutoka Mfuko wa Rais wajasiriamali wa Jimbo la Nyang'hwale ambao hawakupata mkopo huo kwa awamu zote mbili:-

Je, Serikali inawaambia nini wajasiriamali hao katika kipindi hiki kifupi kilichobaki.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

145. MHESHIMIWA RAYNALD ALPHONCE MROPE (MASASI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Utafiti wa matumizi ya gesi ya Mnazi Bay Mtwara unakaribia kukamilika kwa kuonyesha kwamba, kuna gesi yenye ujazo wa 2.6 trilioni cu.ft (tcf) inayoweza kutumika kwa matumizi ya kawaida:-

(a) Je, Serikali inaona ugumu gani kutoa vibali ili miradi mikubwa kama ule wa kusambaza umeme katika Grid ya Taifa ili kutumia MV.300 zinazoweza kuzalishwa Mtwara na kuondoa kabisa matatizo ya umeme nchini na kuanzisha “Compressed Natural Gas”;

(b) Je, kwa kucheleweshe matumizi hayo, Serikali haioni kuwa inadumaza maendeleo ya Ukanda wa Kusini;

(c) Je, ni lini kutakuwa na mpango maalumu wa kuanzisha viwanda

Mtwara ili kutumia vyanzo vya nishati na Madini vilivyopo kwa kutumia Bandari ya Mtwara.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:

146. MHESHIMIWA LUCY THOMAS MAYENGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo:- Mchezo wa ndondi ni moja kati ya michezo yenye kuipa heshima nchi yetu na kuitangaza:-

Je, ni taasisi zipi zinazosimamia shughuli za kuratibu mchezo huo hapa nchini.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

147. MHESHIMIWA DAMAS PASCAL NAKEI (BABATI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Ukanda wote wa Tarafa ya Bashnet kwa muda mrefu hauna kituo cha Polisi hasa ikizingatiwa kuwa Bashnet na Dareda ni Miji inayoibuka kwa kasi kubwa:-

Je, ni lini Serikali itaipatia Tarafa ya Bashnet kituo cha Polisi.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

148. MHESHIMIWA PASCAL CONSTANTINE DEGERA (KONDOA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wilaya ya Kondoa ni moja kati ya Wilaya zilizopangiwa kupatiwa maji kupitia fedha za Mradi wa Benki ya Dunia:-

Je, kwa nini mradi huo umechelewa kuanza na sasa utaanza kutekelezwa lini.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

149. MHESHIMIWA PROF. IDRIS ALI MTULIA (RUFIJI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Wilaya ya Rufiji ni kubwa sana lakini haina majengo ya Mahakama na nyumba za Mahakimu:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga majengo ya Mahakama na nyumba za Mahakimu;

(b) Je, Wilaya ya Rufiji ina Mahakimu wangapi na ina upungufu wa Mahakimu wangapi;

(c) Je, Serikali imesaidia Mahakimu wangapi kutoka Rufiji katika Programu yake ya kujiendeleza (*continuing education).*

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA **DKT. T.D. KASHILILAH**
30 JUNI, 2010 **KATIBU WA BUNGE**